


# Jua sheria

Queensland ina sheria za kukodisha ambazo zinaweza kuwa tofauti na maeneo mengine umewahi kuishi.

Una **haki** na **majukumu** wakati kukodisha. Jua hizo ni nini na epukana na matatizo.

## RTA iko hapa kusaidia

Residential Tenancies Authority (RTA) ni shirika la serikali ambayo inasimamia sheria za kukodisha katika Queensland. Sisi tunatoa msaada na habari kwa wapangaji, makabaila na mawakala wa mali isiyohamishika.

## Matatizo wakati wa kukodisha

Kama wewe na kabaila wako hamuwezi kukubaliana kuhusu jinsi ya kutatua tatizo la kukodisha, sisi tuko hapa kukusaidia kupata ufumbuzi.

RTA inatoa **huduma ya bure ya kusuluhisha mgogoro.**

Tupigie simu kwa 1300 366 311 ili kujua jinsi tunaweza kusaidia.

## Pata habari zaidi za kukodisha

Tembelea tovuti yetu **rta.qld.gov.au** kwa taarifa za kina kuhusu kukodisha katika Queensland.

Tupigie simu kwa **1300 366 311**. Pata majibu ya maswali yako ya kukodisha. Sisi tunafungua Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia 2.30 asubuhi hadi 11 jioni.

## Zungumza lugha yako

Interpreter

Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS) hutolewa bure bila malipo kwa njia ya RTA. tuulize sisi kwa msaada wa kupata mtafsiri wakati wewe unapiga simu, au piga simu TIS moja kwa moja kwa 131 450.

Habari hii ni ya uongozi wa jumla tu. Si ushauri wa kisheria. RTA haiwezi kuhakikisha usahihi au ukamilifu wa taarifa zinazotolewa. Kwa taarifa zaidi rejea kwa *(Sheria 2008 za Wapangaji za Makazi na Malazi ya Vyumba).*

residential tenancies authority

## Baadhi ya sheria za jumla za kukodisha

Wapangaji:

- Lipa kodi ya nyumba kwa wakati
- Weka mahali safi, nadhifu na pasiharibike
- Timiza sheria za mkataba wako wa upangaji
- Heshimu haki za jirani yako ‘kwa amani na utulivu

Landlords:

- Heshimu faragha ya wapangaji na timiza mahitaji ya kuingia
- Fanya matengenezo na marekebisho
- Timiza sheria zote za afya na za usalama
- Weka uhusiano na RTA

Chunguza kanuni kwa habari zaidi

cc BY
Swahili

Creating pathways